

Shift. |

Bus operators prepare for electric buses in major public transport transformation

BY HELLEN
NACHILONGO

Dar es Salaam. Bus operators in Tanzania are preparing for a major shift in the country's public transport sector, with plans to introduce electric buses as early as next year.

The initiative marks a significant step towards greener and more efficient travel for thousands of commuters who depend on long-distance and intercity services.

For Shabiby Company Limited, one of the country's largest fleet operators, the transition is already underway.

The firm's manager, Mr Edward Magawa, told The Citizen that preparations are progressing well as the operator moves towards adopting electric mobility.

Mr Magawa said the company has long maintained a strong partnership with Yutong, a leading bus manufacturer, positioning Shabiby among the brand's largest clients in the region.

This relationship, he noted, has laid the foundation for Shabiby's entry into the electric bus era.

"We are among Yutong's biggest clients, and starting next year, we expect to begin procuring electric buses. We have already placed an order for about 30 units, which are scheduled to start arriving by January," he said.

He added that the arrival of the first batch will signal the start of a trial phase aimed at assessing how the buses perform under Tanzania's diverse road conditions. The company plans to launch test routes linking Dar es Salaam, Dodoma and Arusha—selected for their moderate distances and high passenger traffic.

"We will also test a longer route from Dodoma to Sumbawanga so we can evaluate how the buses perform on rough terrain and in hilly areas," he said.

Mr Magawa added that the trials will help the company adjust operations and ensure passengers continue to enjoy reliable and comfortable services.

We will also test a longer route from Dodoma to Sumbawanga so we can evaluate how the buses perform on rough terrain and in hilly areas

Magawa | Shabiby manager

According to Mr Magawa, Shabiby has invested heavily in preparing for the transition, including staff training and facility upgrades to support the new fleet. He emphasised that passengers should expect the same standard of safety, comfort and quality for which the company is known, even as it experiments with new technology.

The issue of transport fares is also under consideration. Mr Magawa said that because the first

phase will be a pilot, the company will work closely with the Land Transport Regulatory Authority (Litra) to determine appropriate fare structures.

"If the buses prove to be cost-effective, fares are likely to go down, so our customers should be prepared for that possibility," he said.

Director of Kimbinyiko Bus Company, Mr Ferdinand Mabumo, confirmed that his firm also plans to start importing electric buses next year.

Procurement is expected to begin in February, with the first batch due to arrive in May.

"To start with, we will order five buses and gradually expand the fleet as we move forward. Once they arrive, we will then identify the most suitable routes," he said.

Mr Mabumo added that the introduction of electric buses represents a pivotal moment for Tanzania as it looks towards a cleaner and more modern transport future—one that promises enhanced travel experiences and long-term environmental benefits.

NOVEMBA 26>>Ulifanyika mdahalo kuhusu sekta ya usafirishaji ikiwa

Maadhimisho wiki ya usafiri yaleta manufaa

Na REHEMA MAIGALA

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), limesema maadhimisho ya kwanza ya wiki ya usafiri endelevu ardhini, yameleta tija kwa wadau na watumiaji wa usafiri ikiwemo kupata uelewa mzuri kuhusu sekta hiyo.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu Mtendaji wa LATRA CCC, Daudi Daud alisema licha ya kupata uelewa, pia maadhimisho hayo yameleta faida kwa kuzifahamu mamlaka za usafirishaji.

Daudi alisema faida hizo zimetokana na mwitikio mkubwa wa wadau kwa maadhimisho hayo, wakiwamo waliotoka ndani na nje ya nchi ambao walipata fursa ya kubadilishana uzoefu wa matumizi ya

sekta hiyo.

"Mdahalo uliofanyika Novemba 26 mwaka huu, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam, ulikuwa na tija kubwa kwa sababu wadau kutoka nje ya nchi walionesha uzoefu wao huku wadau wa ndani nao wakieleza uzoefu walionao katika sekta ya usafirishaji," alisema.

Pia, Daudi alimpongeza Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Maseke Mabiki kwa kuendeleza bunifu wa njia mbadala katika miji mikubwa ambayo italeta tija kwa sababu hata miji inayoendelea inafanya hivyo.

"Ubunifu wa njia mbadala utasaidia kupunguza foleni katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha," alisema.

Aidha, Daudi alisema maadhimisho hayo yanapaswa kufanyika katika miji yote mikubwa, lengo ni kupata uelewa mzuri kuhusu usafirishaji.

"Binafsi nimeona maadhimisho hayo yalivyofana, hivyo yakiendelea kila mwaka sekta ya usafirishaji itakuwa kubwa huku watumiaji wakielewa vizuri sekta hiyo," alisema.

Hivi karibuni katika kilele cha maadhimisho ya kwanza ya wiki ya usafiri endelevu ardhini, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya uchukuzi, Maseke Mabiki alisema serikali imeendelea kasisitiza dhamira ya kuboresha sekta ya uchukuzi nchini, hatua inayoweza Tanzania kuongoza Afrika kwa urefu wa mtandao wa barabara na kushika nafasi ya tano duniani.

KONA YA JAMII



MWANANCHI.CO.TZ

Latra tupieni macho daladala hizi, Zingiziwa tupatiwe maji

Daladala zinazokatisha ruti zinasababisha usumbufu kwa abiria, kuongeza gharama na muda wa safari. ni Muhimu mamlaka husika zichukue hatua ili kukomesha tabia hiyo.

Msomaji

Wizara ya Maji, tunaomba mtuambie ni lini hasa wakazi wa Zingiziwa tutafikiwa na maji ya bomba kwani ni muda sasa tunatumia maji ya visima vinavyochimbwa kwa msaada wa mashirika ya dini.

Shani

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (Latra), siku hizi daladala za Kawe-Segerea zimepungua sana, jambo linalotupa adha wasafiri. Tunaomba kujua shida ni nini.

Filbert

Wakati michango ya sherehe zikiwamo harusi ikishamiri miezi hii, pia tusiwasahau watoto wanaotakiwa kwenda shule mwakani na familia zao hazina uwezo kuwachangia pia.

Joel

Naomba kujua nani wanahusika haswa katika kukagua vituo vya kukaa abiria wakisubiri usafiri, hasa maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ambapo vingi kwa sasa vinaonekana ni mali ya wafanyabiashara wadogo waliovigeuza maduka na majiko.

Leonard

Kuna baadhi ya watoa dawa hospitali hawatoi maelekezo vizuri kwa wagonjwa, unaweza

kukuta anamwambia atumie dawa kutwa mara tatu, badala ya kukueleza kunywa bila baada ya saa ngapi.

Msomaji

Haya malalamiko ya kupata mikopo kihalisia yapo, kuna haja ya watendaji kufuatilia kiundani, nani hasa ni vikwazo katika kutimiza dhamira njema hiyo ya Serikali katika uwezesaji wananchi kiuchumi.

Mage

Kipindi hiki cha likizo pia tukumbuke kuwapeleka watoto katika mafunzo ya dini kutokana na muda wao mwingi kuutumia wakiwa shuleni.

Leila

Makondakta na madereva wa kituo cha Mwenge hamzitendei haki sare zenu nzuri mlizobuniwa, kwani kwa muda mfupi tayari baadhi yenu mmeonekana kutoziji na ule usafi kuondoka.

Kenny

Madalali, mnapowatafutia watu nyumba jitahidini kuwa wakweli badala ya kufikiria kupata tu hela ya mguu, kwani wengi huwapeleka kwenye nyumba ambazo tayari zina mpangaji au kulipisha hela ya usafiri kabla ya kuona nyumba.

Imma

Hizi pikipiki zinazotembea barabarani na kuwa na mlio kama risasi inalipuliwa, tunaomba kikosi cha usalama barabarani mtuambie kama zinaruhusiwa kwa kuwa zimekuwa nyingi na zinashtua watu zinapopita. **Joe**

Suala la mikesha ya sherehe mtaani inayofungulia muziki kwa sauti linaonekana kuwa donda ndugu, kwani miziki hiyo inapigwa hadi kunakucha na hakuna hatua zinazochukuliwa na viongozi.

Jebra

Tunaomba viongozi, mkipewa madaraka, fanyieni kazi kero za wananchi kwani kuna zinazoumiza sana, na mkumbuke mnapewa nafasi hizo ili kuwahudumia na kuwasaidia wananchi kwa uadilifu.

Gamiela

Kauli ya Wasira kuhimiza kupata haki kwa njia za amani ni ujumbe muhimu kwa jamii ya vijana, hususan katika kipindi cha changamoto za kisiasa.

Zuwena

Kuongeza kasi ya kutatua malalamiko ya maji kwa wananchi kunalenga kupunguza adha, hususan kwa wanawake na watoto wanaobeba mzigo wa kutafuta maji.

Philipo

Ushauri wa waziri kwa tume kufanya uchunguzi wa kina unaonesha umuhimu wa kuzingatia ushahidi kabla ya kutoa taarifa kwa umma.

Juma

Ushirikiano wa viongozi na tume ya maadili unaongeza uwajibikaji na kuimarisha mfumo wa kisheria wa kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka.

mwananchi

Vijana, nawakumbusha dunia ya sasa ina taarifa nyingi, mitazamo mingi, na sauti nyingi zinazoshindana kushawishi fikra zetu, ila si kila taarifa ni sahihi.

Kibua

Licha ya yanayoendelea, inasikitisha polisi bado wanaendelea na ratiba zao za kuwachukua watu kimyakimya, hii inaonesha nidharaukwawwananchi na inaonesha wanajiamini hakuna tutakachoweza kuwafanya.

Chalzhidee

Mtaa wa Mburahati, jijini Dar es Salaam, haujapata maji zaidi ya miezi mitatu, mbaya zaidi tunaona yakitoka kwingine ila huku kwetu hayafiki kabisa.

Idda Mkoba.

Viongozi wa dini ni sehemu muhimu ya kujenga umoja na utangamano wa wananchi, hivyo ni muhimu kwao kuishauri Serikali na viongozi kwa utaratibu unaojenga na si kubomoa.

Mishosha-7

Katika kipindi hiki ambacho amani ndiyo inahubiriwa na viongozi, kuna haja pia wakaenda kutoa pole kwa wafiwa na kutembelea familia zao kuwafariji.

Angel

Maeneo ya Chanika, umeme umekuwa ukikatika hata kwa siku mara tano, hii inatuweka hatarini wananchi kuunguza vifaa vyetu vya umeme na sisi tunaotekeleza biashara zetu kwa kutegemea uwepo wa umeme kupata hasara.

Catherine